

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 1

32 Gideoni apiga Wamidiani

Kwa Biblia Waamuzi mlango wa 7

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hujibu maombi. Watu wachache wanaweza kufanya mambo makubwa Mungu akiwasaidia.

Somo

Waisraeli waliabudu Mungu kwa miaka arobaini baada ya kuwaokoa kutoka kwa Wakanaani. Waisraeli walikuwa na amani kutoka kwa adui wao. Baadaye walishau Mungu tena. Walianza kuabudu sanamu tena. Hawakuuliza Mungu awalinde.

Wamidiani walikuwa adui wa Waisraeli. Walikuja na kushambulia Waisraeli. Wamidiani walikuja na kuharibu mimea na kuiba mifugo yao. Waliharibu nyumba za Waisraeli. Kwa miaka saba Wamidiani waliteza Waisraeli. Waisraeli walitoka nyumbani kwao na kuenda kujificha kwa mapango na kwa tundu za milima. Wamidiani waliharibu kila kitu.

Baadaye Waisraeli walikumbuka vile Mungu alikuwa amewasaidie. Waliomba Mungu tena. Waliacha kuabudu sanamu. Waliuliza Mungu awasamehe uovu wao. Waliomba Mungu awasaidie na awaokoe kutoka kwa Wamidiani.

Mungu alichagua mtu aliyeitwa Gideoni ili aongoze Waisraeli. Mungu aliahidi kusaidia Gideoni ashinde Wamidiani.

Maswali

1. Adui wa Waisraeli walikuwa nani?
2. Mbona Mungu hakulinda Waisraeli?
3. Waisraeli waliporudia Mungu, nani alichaguliwa kuwaongoza?
4. Jeshi la Wamidiani lilikuwa na watu wangapi?
5. Mbona Mungu alisema Gideoni alikuwa na watu wengi sana?
6. Mwishowe Gideoni alikuwa na watu wangapi?
7. Gideoni alisikia nini kwa kambi ya Wamidiani?
8. Gideoni aligawanya watu wake kwa vikosi vingapi? Alimpa kila mtu nini?
9. Watu wa Gideoni walifanya nini?
10. Wamidiani walifanya nini?

Majibu

1. Wamidiani walikuwa adui wa Waisraeli.
2. Watu waliabudu sanamu badala ya Mungu.
3. Mungu alichagua Gideoni kuongoza Waisraeli.
4. Wamidiani walikuwa wengi na ilikuwa vigumu kuwahesabu.
5. Mungu ndiye angeokoa Waisraeli. Gideoni hakutakiwa kuwa na watu wengi.
6. Gideoni alikuwa na watu 300.
7. Mtu alikuwa anasema ndoto zake. Mkati wa shayiri uligonga na kuangusha hema. Mtu mwingine alisema hiyo ilimaanisha Gideoni atashinda Wamidiani.
8. Vilikuwa vikosi 3. Aliwapa tarumbeta, taa na mitungi.
9. Walipiga tarumbeta, wakavunja mitungi na kubeba taa juu.
Walipasa sauti, "Upanga wa Bwana na wa Gideoni."
10. Walifikiri Gideoni alikuwa na jeshi kubwa. Walipigana wenyewe kwa wenyewe. Walitoroka.

Jeshi la Midiani lilikuja kushambulia Waisraeli. Wamidiani walikuwa wengi sana na hawangeweza kuhesabiwa. Walipiga kambi upande moja wa bonde. Gideoni na jeshi la Israeli walipiga kambi upande mwingine wa bonde. Kulikuwa na wanaume 32,000 kwa jeshi la Gideoni. Jeshi la Waisraeli lilikuwa na watu wachache ukulinganisha na jeshi kubwa la Wamidiani.

Mungu alimwambia Gideoni kwamba jeshi lake lina watu wengi sana. Mungu atashindia Waisraeli vita. Hawakutakiwa wawe watu wengi. Gideoni aliambia watu waliokuwa waoga warudi nyumbani. Watu 22,000 walirudi nyumbani kwa sababu walikuwa waoga. Gideoni alibaki na watu 10,000 kwa jeshi lake. Mungu aliambia Gideoni kwamba alikuwa bado ana watu wengi sana. Mungu aliambia Gideoni apeleke watu wake mtoni wakunywe maji. Watu mia tatu waliramba maji kutoka kwa mikono yao. Wengine wote walipiga chini magoti ili wanywe. Mungu alichagua watu mia tatu walioramba maji. Aliambia Gideoni arudishe watu wengine nyumbani. Gideoni alibaki na jeshi la watu mia tatu. Alikuwa na watu mia tatu kupigana na maelfu ya Wamidiani. Gideoni alitakiwa kuamini kwamba Mungu atawasaidia.


Jioni hiyo Mungu aliambia Gideoni ateremke chini kwa kambi ya Wamidiani. Gideoni alinyemelea polepole katikati ya mahema. Nje ya hema moja, Gideoni alisikia watu wakijadiliana. Mmoja wao alisema, "Usiku wa jana niliota. Mkate wa shayiri ulianguka kambini. Ulipiga hema na hema ikauanguka chini." Rafiki yake alijibu, " Hii ina maanisha ni upanga wa Gideoni. Yeye ni Mwisraeli. Mungu atamsaidia ashinde Wamidiani."

Gideoni alitiwa moyo aliposikia hivyo. Alikuwa na imani kwamba Mungu atamsaidia ashinde Wamidiani. Gideoni alirudi kambini mwa Waisraeli. Aliwasanya watu wake pamoja. Waliomba Mungu. Waliuliza Mungu awasaidie. Gideoni aliambia watu wake, "Msiogope Mungu atatusaidia tushinde Wamidiani."

Gideoni aligawanya watu wake kwa vikosi vitatu vya watu mia moja kila kimoja. Alipea kila mtu tarumbeta, taa na mtungi. Aliwambia chenye watafanya.

Watu wa Gideoni walifunika taa zao na mitungi ili mwangaza usionekane na mtu yeoye. Wale watu mia tatu walienda kimya polepole, wakafuka bonde mpaka kwa kambi ya Wamidiani. Watu wa Gideoni walitawanyika na kuzunguka kambi ya Wamidiani. Kila kikosi kilienda upande wake. Walikaa na kungoja ishara kutoka kwa Gideoni.

Wamidiani walikuwa wamelala fofoto. Walinzi wachache wa Wamidiani walitembea juu na chini kwa giza. Walikuwa wakitafuta Waisraeli. Waisraeli walichifija msituni wakingojea ishara ya Gideoni.



Bunde tu,
Gideoni akaruka
na kusimama.
Watu wake nao
wakafanya
hivyo.

Wakapika tarumbeta kwa mlion wa juu. Wakavunja mitungi kwa vishindo. Mwangaza wa taa ulimlika kambi ya Wamidiani yote. Walipika tarumbeta tena na kusema kwa sauti, " Upanga wa Bwana na wa Gideoni."

Wamidiani waliamka kutoka kwa usingizi. Walichanganyikiwa kwa kelele na mwangaza. Walikimbia kutoka kwa mahema. Walisikia kelele yote ya tarumbeta na ya watu. Waliona mwangaza uliozunguka kambi yao. Mungu alifanya Wamidiani wafikirie kwamba Gideoni alikuwa na jeshi la kupigana nao. Gideoni na watu wake waliwaangalia tu. Kulikuwa na kelele mingi kambini. Kwa sababu ya giza na kuchanganyikiwa, Wamidiani walianza kupigana wenyewe kwa wenyewe. Vita viliendelea kambini. Wamidiani waliogopa na kutoroka. Walitoroka wote.

Gideoni na watu wake mia tatu walifukuza Wamidiani na kuua watawala wao wawili. Wamidiani walitoroka kutoka kwa Gideoni. Mungu aliokoa Waisraeli kutoka kwa Wamidiani. Waisraeli waliamini na kuabudu Mungu tena. Mungu aliwapa amani kutoka kwa adui wao kwa miaka arobaini.